Watafiti wa UVMMC Wanajiunga na Utafiti wa Taifa Unaotathmini Udhibiti Salama wa Maumivu kwa Majeshi na Raia Waliojeruhiwa.

Watafiti kwenye Chuo Kikuu cha Vermont wanashiriki katika Jaribio la Mkakati wa Kutumia Analgesia Kabla ya Kufika Hospitalini (PAIN) linalofanywa na Chuo Kikuu cha Pittsburgh na kufadhiliwa na Idara ya Ulinzi. Utafiti unalinganisha ufaafu na usalama wa dawa mbili zinazotumiwa sana kutibu maumivu baada ya jeraha kwa majeshi na raia.

Dawa mbili ni Fentanyl, opioidi na Ketamine ya dozi chache, nusukaputi. Utafiti, utakaoanza majira ya majani kupukutika ya 2024 unaongozwa na Daniel Wolfson, Mkurugenzi Msimamizi, Profesa Mshirika wa Tiba ya Dharura na Ajai Malhotra, Mkurugenzi Msimamizi, Profesa wa Upasuaji na Mkurugenzi wa Matibabu ya Kiwewe wa Kituo cha Kiwewe cha Daraja la I huko UVMMC.

Sasa, dawa zote mbili zinatumiwa huko Vermont na watoa huduma wa kabla ya kuenda hospitalini ili kuondoa maumivu baada ya jeeraha. Hata hivyo, bado hatujui dawa inayofaa zaidi kuondoa maumivu na salama kwa kuepuka madhara mabaya au hatari. Utafiti utasaidia kujibu maswali haya na utakuwa wa manufaa kwa majeshi yaliyojeruhiwa nyanjani na raia kwa jumla, ikiwa ni pamoja na wakazi wa Vermont. Utafiti ni mmoja wa mfululizo wa tafiti zinazofadhiliwa na Mtandao wa Idara ya Ulinzi kupitia Kuhusisha Chunguzi katika Huduma za Kiwewe na Dharura (LITES – www.litesnetwork.org) ili kupata miongozo ya desturi za matibabu na kubadilisha viwango vilivyopo vya utunzaji wa majeraha ya kiwewe.

“Fentanyl hutumiwa sana kutibu maumivu kwa wagonjwa wa kiwewe lakini inaweza kupunguza viwango vya oksijeni na shinikizo la damu, hivyo kuweza kufanya hali ya mtu aliyejeruhiwa kuwa mbaya zaidi na wakati mwingine kuhitaji tyubu ya kupumulia. Pia kuna hatari ya uraibu wa muda mrefu wa opioidi. Ketamine ya dozi chache ni faafu kwa kudhibiti maumivu na inaweza kupunguza hatari zinazohusishwa na opioidi, lakini inaweza kusababisha madhara kama vile njozi, wasiwasi na kuhisi kujitenga,” alisema Dkt. Wolfson. Tatizo hili ni kubwa katika jeshi. “Lengo ni kusaidia jeshi kutoa utunzaji bora kwa watumishi wetu waliojeruhiwa, kwa kuamua dawa faafu zaidi ya kuondoa maumivu na pia ile iliyo na madhara kidogo mabaya ya muda mfupi na ya muda mrefu.” Dkt. Malhotra aliongeza.

Utafiti utawaandikisha takribani wagonjwa 1000 waliojeruhiwa kutoka kwenye vituo kumi na viwili vikubwa vya elimu ya matibabu nchini Marekani ambavyo ni sehemu ya Mtandao wa LITES. Wagonjwa hawa walioandikishwa watachaguliwa kwa kukisia kupokea Fentanyl au Ketamine ya dozi chache kwa ajili ya kuondoa maumivu baada ya jeraha. Wagonjwa wote walioandikishwa watafuatiliwa kwa uangalifu kwa ajili ya ufaafu wa kuondoa maumivu na matatizo ya muda mfupi na muda mrefu. “Ketamine na Fentanyl tayari zinatumiwa na Huduma za Matibabu ya Dharura huko Vermont kama tiba wastani ya udhibiti wa maumivu. Utafiti huu

utatusaidia kutambua dawa inayotoa utunzaji bora huku ikipunguza hatari,"
Dkt, Wolfson alibaini.

Yeyote anaweza kujiondoa kwenye utafiti kwa kuwasiliana na timu ya utafiti kwa nambari 1-800-664-0557 au kutuma baruapepe kwa PAINStudy@edc.pitt.edu ili kupokea bangili ya kujiondoa ya "Utafiti wa HAKUNA MAUMIVU". Kwa taarifa zaidi tembelea www.ClincialTrials.gov na urejelee NCT05437575. Ni muhimu kwa wakazi wa Vermont kuelewa kwamba kujiondoa hakutazuia wagonjwa waliojeruhiwa kupokea dawa ya maumivu kulingana na kiwango cha utunzaji, kwa kujiondoa katika uandikishaji kwenye utafiti pekee.

Utafiti huu unafadhiliwa na Idara ya Ulinzi (DoD) mkataba W81XWH-16-D-0024 W81XWH-19-F-0539. Maoni au mapendekezo yoyote yanayotolewa katika makala haya ni ya mwandishi na hayawakilishi mitazamo ya Idara ya Ulinzi.